
# SURUA



**Surua ni ugonjwa unaosababishwa na virusi vya surua. Surua huanza na homa, kutokwa na kamasi, kikohozi, macho mekundu na koo kuuma. Kisha hufuatwa na upele unaoenea mwilini kote. Ugonjwa wa surua unaweza kusababisha maambukizi ya masikio na kuendesha. Madhara makubwa yanaweza kutokea kutokana na ugonjwa wa surua. Baadhi ya watoto wanaweza kupata maambukizi kwenye mapafu (nimonia) au uvimbe wa ubongo, ambao wakati mwingine unaweza kusababisha kifo.**

**Iwapo unashuku kuwa mtoto wako ana ugonjwa wa surua, pigia mtoa huduma wako wa afya simu mara moja.**

**Hakikisha kuwa unamweka mtoto wako mbali na watu wengine wakati anaugua.**

## Je, ugonjwa huu huenezwa aje?

- Surua ni virusi vinavyoweza kuenea kwa urahisi kutoka mtu mmoja hadi mwingine.
- Virusi hivi ni miongoni mwa magonjwa yanayoenea kwa urahisi zaidi. Huenea hewani kupitia matone ya mate. Huenea mtu aliye mgonjwa huo anapokohoa au kupiga chafya.
- Virusi vya surua vinaweza kubaki hewani kwa hadi saa mbili baada ya mtu aliye mgonjwa kuwa ndani ya chumba hicho.
- Watu walioambukizwa wanaweza kusambaza surua kwa wengine kuanzia siku nne kabla hadi siku nne baada ya upele kujitokeza.

## Je, dalili zake ni zipi?

- Kutokwa na kamasi
- Homa kali (inaweza kuzidi 104°F)
- Uchovu
- Kikohozi
- Macho mekundu, yenye majimaji, au konjunktivaitisi ("macho yenye rangi ya waridi")
- Upele wenye rangi nyekundu wenye vinundu unaoanza mahali nywele za kichwa zinaanzia na kuenea hadi mikononi na miguuni kati ya siku tatu hadi tano baada ya dalili kuanza

## Je, ugonjwa wa surua unaweza kuzuiwa aje?

*Njia bora ya kuepuka kupata ugonjwa wa surua ni kupata chanjo!*

- Chanjo ya MMR hulinda dhidi ya surua, matumbwitumbwi na rubella.
- Dozi mbili za chanjo ya MMR zinahitajika kwa ulinzi kamili. Dozi ya kwanza inapaswa kutolewa mtoto akiwa na umri wa miezi 12 hadi 15 na dozi ya pili akiwa na umri wa miaka 4 hadi 6.
- Watoto wenye umri wa miezi 12 hadi miaka 12 wanaweza kupata chanjo ya pamoja ya MMRV, ambayo pia hulinda dhidi ya varicella (tetekuwanga).

*Matineja na watu wazima wanapaswa pia kuwa wamepokea chanjo zao. Hakikisha umewasiliana na mtoa huduma wako wa afya kuhusu kupata chanjo dhidi ya ugonjwa wa surua.*

**Kwa maelezo zaidi kuhusu chanjo, tafadhali tembelea: https://www.cdc.gov/vaccines/hcp/vis/vis-statements/mmr.pdf**

**BUREAU OF COMMUNICABLE DISEASES**
https://www.dhs.wisconsin.gov/dph/bcd.htm | DHSDPHBCD@dhs.wi.gov
Wisconsin Department of Health Services | Division of Public Health
P-42174SW (03/2017)